# MWONGOZO WA MAFUNZO YA VINARA WA MABORESHO ENDELEVU KWA VITENDO KUPITIA MKAKATI WA QUADS1[1]

## HALMASHAURI ZA TANDAHIMBA, MASASI,

## MASASI MJI NA NEWALA MJI

## December, 2019

*Scientists QUADS Project: Abdallah, G., Mkumbo, E., Zamoyoni, J., Mlaguzi,M., and Manzi, F. 2019*
*Ifakara Health Institute, P.o. Box 78373, Dar es Salaam Tanzania*

**Acknowledgements:**

This work was carried out with the aid of a grant from the Innovating for Maternal and Child Health in Africa initiative- a partnership of Global Affairs Canada (GAC), the Canadian Institutes of Health Research (CIHR) and Canada's International Development Research Centre (IDRC)

[1] Quality Improvement in Maternal and Newborns Health At District Scale (QUADS).
Mkakati wa kuboresha kuduma  ya Afya ya mama na mtoto katika ngazi ya Wilaya

**NAFASI YA KINARA KATIKA MABORESHO ENDELEVU**

1. **Nani ni KINARA wa maboresho endelevu?**

    ***Ni mtu ambaye ana uwezo wa kubuni fikra za mabadiliko yenye tija, kushawishi, kuongoza, kutekeleza na kueneza mabadiliko hayo ndani mifumo ya utendaji kazi katika taasisi/jumuiya/ idara au mifumo.***

2. **Maeneo yapi KINARA anaweza kuhusika kuleta maboresho endelevu?**
    a. **Afya – hususani afya ya mama na mtoto**
    b. **Mambo ya maendeleo – mfano katika elimu, maji, uchumi**

3. **Kazi za KINARA wa maboresho endelevu ya huduma**

    Majukumu makubwa ya **Kinara** wa maboresho endelevu ni;
    a. Kubuni na kutekeleza na kusimamia mabadiliko yenye kuleta tija
    b. Kuhamasisha na kuwashirikisha wengine katika kutekeleza na kuendeleza mabadiliko

4. **Kwanini tunahitaji KINARA wa maboresho endelevu?**
    1. Ni mtu muhimu katika kusaidia ubunifu mpya, kuboresha, kueneza/kutekeleza na kusimamia juhudi za kuleta mabadiliko yenye tija katika hatua za uanzishaji, uendelezaji na kusimamia fikra za mabadiliko ya maboresho.
    2. Kupunguza gharama za kutumia vinara/ wataalamu wa nje katika kuleta ubunifu mpya, kueneza, kutekeleza na kusimamia juhudi za kuleta mabadiliko yenye tija.

5. **Sifa/vigezo vya kuchagua KINARA wa maboresho endelevu**

    a. Ana uwezo wa kushawishi na kuwasiliana kwa wengine
    b. Ana uwezo wa kufundisha wengine na kufanya usimamizi
    c. Ana uwezo wa kuhamasisha rasilimali ndani na nje ya eneo la kazi
    d. Ana uwezo wa kujituma bila kusimamiwa au kulazimishwa katika kuleta mawazo mapya katika kuleta au kutekeleza mabadiliko
    e. Awe ni mwenye kukubalika na kukubali wengine, kuheshimika na kuheshimu wengine
    f. Ni muhusika wa ndani wa taasisi/idara/ mfumo

**Sifa nyinginezo**

**a.** Uwakilishi wa kanda ndani ya Wilaya/Halmashauri, Tarafa na Kata

**b.** Uwakilishi wa vituo: Hospitali, Vituo vya afya na Zahanati.

**c.** Kwa zahanati, msisitizo ni katika zahanati zenye kuhudumia watu wengi zaidi/ idadi kubwa ya akina mama kujifungua.

**MAANA NA SIFA ZA MABORESHO ENDELEVU**

**1. Utangulizi:**

**Maana ya maboresho endelevu** *Ni mfumo wenye kufuata hatua maalumu ambazo hupelekea kuleta maboresho endelevu ya jambo lolote. Kuzijua hatua hizi na namna ya kuzitumia ni muhimu sana ili kuweza kuleta maboresho endelevu.*

Maboresho endelevu huanza na mtu ambae ni mimi baada ya kuelewa kwa kina shina la tatizo lenyewe. Maboresho endelevu yanatarajiwa kuwepo katika maeneo yote yanayotuzunguka. Mabadilko ya mtu mmoja yanaweza kuleta tofauti kubwa katika kikundi/taasisi/jamii/idara. Ni muhimu kuzingatia kuwa maboresho huanza na mimi mwenyewe, kwa kukubali kubadilika, na baadaye kubadilisha wengine. Maboresho endelevu huanza kwa kutumia rasilimali zilizoko katika eneo lako, ambazo hupunguza gharama na muda. Na kama nafasi ikiruhusu, mahitaji mengine makubwa yanaweza kupatikana kutoka ngazi tofauti katika kuongeza tija na matokeo makubwa zaidi.

**2. Lengo Kuu**

- Utendaji bora unaotokana na matumizi sahihi ya mbinu za uboreshaji endelevu katika maeneo mbalimbali ya maisha, ili kuleta
  - Ufanisi na utendaji bora
  - Kiwango cha juu cha matokeo ya ubora uliotukuka katika huduma

**3. Malengo Mahususi**

- Kueleza maana ya uboreshaji endelevu *mfano* katika eneo la afya ya mama na mtoto
- Kutambua umuhimu wa matumizi sahihi na uchambuzi wa takwimu katika maboresho endelevu
- Umuhimu wa mawasiliano mazuri na ushirikishwaji katika maboresho endelevu

**4. Je maboresho endelevu yana umuhimu?**

a. Kuimarisha kwa kiwango cha hali ya juu kimaisha na utendaji kupitia mtu mmoja na, au katika makundi ya watu, taasisi, jumuiya au idara.

b. Ubora wa kiwango cha chini unasababisha matatizo na gharama kubwa
c. Yanaongeza ari na moyo wa kufanya kazi kwa mtu au taasisi
d. Kuleta maendeleo kwa ujumla wake katika nyanja zote za kimaisha

**5. Namna ya kufikia maboresho endelevu.**

Maboresho endelevu hufikiwa kwa kutumia mbinu za maboresho, zikiwemo mawasiliano na ushirikishwaji wa TIMU. Maboresho hayo hufikiwa kwa haraka na ufanisi zaidi kupitia njia ya kufanya kazi kwa TIMU, kwa sababu:

a. Unajifunza zaidi katika timu kwa pamoja
b. Ni vigumu kufanya maboresho peke yako
c. Unahitaji maoni ya watu wengine
d. Unahitaji ujuzi tofauti tofauti kwa wengine
e. Unahitaji suluhisho/maamuzi kwa pamoja na wengine
f. Utahitaji watu wa kukukosoa, ushauri na kukuelekeza.

**6. Mambo yanayohitajika kufikia maboresho yaliyo bora na endelevu**

a) Mawasiliano yenye mrejesho
b) Mazingira wezeshi
c) Uongozi Imara na wenye kujitoa na kujituma
d) Matumizi ya kanuni na miongozo ya kazi kuhusu maboresho
e) Matumizi sahihi ya Takwimu

# SAYANSI YA MABORESHO

**Hatua kwa Hatua**

## Sayansi ya maboresho ni nini?

***Mkufunzi anza kwa kuwauliza washiriki wanaelewa nini maana ya maboresho? Sikiliza bila kukosoa japo unaweza kuhoji zaidi kupata ufafanuzi kisha wape tafsiri rasmi ya sayansi ya maboresho.***

Ni mfumo wenye kufuata **hatua maalumu** ambazo hupelekea kuleta maboresho endelevu ya jambo lolote. Kuzijua hatua hizi na namna ya kuzitumia ni muhimu sana ili kuweza kuleta maboresho endelevu.

***Leo katika somo letu tunajifunza hatua za kupitia ili kuweza kufanya maboresho. Unaanzia wapi na unaishia wapi.***

# HATUA YA KWANZA

## KUBAINI TATIZO/CHANGAMOTO

Maboresho yoyote huanza baada ya **kugundua tatizo/changamoto**

Bila kugundua changamoto hakuna uwezekano wa kufanya maboresho

***Hii inawezekana kweli? Eti unasema mwaka huu ninapanga kufanya maboresho makubwa, halafu ukiulizwa maboresho ya nini? Unasema, hata sijui ya nini. Ni wazi utaonekana una kasoro, ni lazima ujue changamoto kwanza***

## Mbinu gani hutumika ili kugundua tatizo /changamoto?

Kuangalia takwimu kunakusaidia kujua kama kuna tatizo linalohitaji maboresho

**Kama hakuna takwimu, hakuna uwezekano wa kugundua tatizo (***Mali bila daftari hupotea bila habari).* **Takwimu (sahihi) ni moyo wa maboresho yoyote**

Mfano: Takwimu kuonyesha-Kupungua kwa mavuno, mahudhurio ya mikutano, makusanyo ya ushuru nk- **Uchambuzi wa takwimu huashiria changamoto inayohitaji maboresho**

***Haya Sasa baada ya kugundua tatizo/ changamoto ni hatua gani inafuata?***

# HATUA YA PILI

## KUBAINI CHANZO CHA TATIZO/CHANGAMOTO

*Hongera sana kwa kubaini tatizo katika hatua ya kwanza*

Hatua hii sasa ni ya kujifunza kubaini chanzo cha tatizo. Wengi wetu tumekuwa tukikosea sana, tunatumia nguvu nyingi kutatua **matokeo** ya tatizo kuliko kutatua **chanzo** cha tatizo, na hii hupeleka tatizo kuendelea kujirudia kila mara.

**Mbinu gani hutumika kubaini chanzo cha tatizo/changamoto?**

Kuna mbinu za aina nyingi kubaini chanzo cha tatizo. Kwa hapa tutatumia njia ya mwiba wa samaki.

**Mwiba wa samaki (Fishbone) -** Hii ni mbinu inayotumika kusasambua changamoto hadi kubaini CHANZO CHA TATIZO

**Hatua za kutengeneza mwiba wa samaki**

1. Weka (chora) kichwa ambacho huwakilisha tatizo/changamoto ulilolibaini katika hatua ya kwanza.

**Mfano; Tatizo -Makusanyo hafifu ya mapato ya Kijiji**

**(**Kisha weka mwiba mkuu wa kati wa samaki)

2. Weka Miiba midogo ikianzia kwenye mwiba mkuu- ambayo huwakilisha **aina kuu za sababu** zinazopelekea tatizo lililopo


**Mfano; Aina kuu za sababu- Ujuzi wa kutunza fedha, Uchache wa biashara, Hali ya hewa**

3. Katika kila **aina ya sababu kuu** uliyoiweka hapo juu (hatua ya 2), weka **visababishi vya sababu kuu** husika (cause) inayopelekea tatizo hilo


**Mfano: Sababu kuu - Ujuzi mdogo kutunza fedha**

**Kisababishi (cause) - Hakuna mhasibu aliyesomea**

**Umbo 1: Mfano wa mwiba wa samaki**




Umbo 2: Mfano wa mwiba wa samaki1[2]




***Baada ya kuchambua na kubaini sababu/visababishi (causes) kwa kila aina ya sababu kuu….NINI HATUA GANI INAFUATA TENA?***

[2] http://www.wallStreetMojo.com

# HATUA YA TATU

## KUCHAMBUA NA KUPIMA VISABABISHI (CAUSES) VYA SABABU KUU ZA TATIZO/CHANGAMOTO

**Nadhani umegundua kitu kwamba**, katika kila aina ya sababu **kuu**, kuna visababishi (**causes**) vingi na hapo ndipo tunapotumia mbinu nyingine zaidi kuona ni visababishi vipi vyenye nguvu zaidi. Ili kupata ufanisi ni vema kutatua visababishi vyenye mchango mkubwa zaidi kuliko kuweka jitihada kwenye kutaka kutatua kila kisababishi.

***Sasa ni mbinu gani inatumika kuweza kupima na kubaini visababishi vyenye nguvu zaidi kati ya vingi vinavyochangia uwepo wa sababu kuu?***

Kanuni ya PARETO1[3] ambayo pia hujulikana kama kanuni ya 80/20

Kabla ya ufafanuzi wa nini maana ya hii kanuni hebu soma sentensi hizi, utapata picha

- 80% ya mauzo ya kampuni hutoka kwa 20% ya wateja kati ya wateja wote waliopo.
- 80% ya ardhi yote ya nchi ya Italia (kipindi hicho cha nyuma) ilikuwa inamilikiwa na 20% tu ya wananchi wote wa Italia
- 80% ya mafanikio ya timu Fulani yanachangiwa na 20% ya wachezaji.

Mchumi huyu **Vilfredo Pareto** alikugundua uwiano wa aina hii na kanuni hii imekuwa ya msingi sana kwenye sayansi ya maboresho.

**Kwamba** 80% ya Sababu kuu inayopelekea tatizo au changamoto, husababishwa na 20% tu ya **visababishi** kati ya vyote vilivyopo.

Kwa msingi huu, kanuni hii inatutaka tubaini **visababishi vikuu** kati ya vyote vilivyopo na kuweka nguvu kutatua visababishi hivyo vyenye mchango mkubwa kwenye tatizo/changamoto.

**Maana yake nini?**

Ukitazama visababishi hivyo utagundua vipo vichache vinavyobeba vingine (**visababishi vikuu**)

**TUMIA KANUNI HII KUVIBAINI NA KUVIORODHESHA!.**

**SASA NINI KINAFUTA SASA BAADA YA KUBAINI VISABABISHI VIKUU?**

---

[3] https://en.wikipedia.org/wiki/Pareto_principle

# HATUA YA NNE

**KUBAINI MIZIZI (ROOTCAUSE) WA VISABABISHI VIKUU**

**Hongera!**

Baada ya kutumia kanuni ya 80/20 maana yake umebakiwa na **visabibishi vikuu** (Main Causes) vile vyenye mchango mkubwa zaidi kwenye sababu kuu

Nini kinafuata tena?

Kwa kila kisababishi kikuu, kuna kazi ya kutafuta **MZIZI HASA WA KILA KISABABISHI KIKUU**

## *Hili sasa hufanywa kwa kutumia hii kanuni ya Maswali 5 (5 WHYS).*

Kanuni hii hufanyaje kazi?

Mfano; kisabishi kikuu cha mapato duni ni **uwezo mdogo wa wahasibu**. **Kwa hiyo,** t**unapaswa kutafuta mzizi wa kisababishi hiki kwa kujiuliza maswali 5**

**Mfano:**

Why 1 : **Kwanini wahasibu wana uwezo mdogo?**

- Jibu- Kwa sababu hawakusomea

Why 2: **Kwa nini hawakusomea?**

- Jibu-Sababu hatukuwasomesha

WHY3**: Kwanini hamkuwasomesha?**

- Jibu- Sababu hatukuwa na pesa?

WHY 4: **Kwanini hamkuwa na pesa?**

UKIFIKA MAHALI AMBAPO UNAONA JIBU NI LA MWISHO, HAPO MKAKATI WA KUTATUA TATIZO UNAWEKWA KUZINGATIA JIBU LA MWISHO**- NA HUO NDIO MZIZI HASA WA KISABABISHI KIKUU CHA SABABU KUBWA YA TATIZO /CHANGAMOTO**

Zingatia: Maswali ya kidadisi yanaweza kuwa 5 au pungufu ya tano au zaidi ya tano, itategemea.

LAKINI?

| |
|---|
| KUJUA MIZIZI YA TATIZO TU KUNATOSHA KULETA MABORESHO? |

## *Hapana*!!

### NI UTAFUTAJI NA UTEKELEZAJI WA MIKAKATI YA KUTATUA MIZIZI YA TATIZO

# HATUA YA TANO

## KUBAINI MIKAKATI YA KUTATUA MIZIZI YA VISABABISHI VIKUU VYA TATIZO

Hii sasa ni hatua muhimu mno na safari ya hatua zote zilizotangulia lengo kubwa ni kufika hapa, kubaini mizizi ya visababishi vikuu.

Kwa hatua hii, timu ya maboresho sasa inapaswa kujadili kwa pamoja ni mikakati gani inaweza kutumika kutatua mizizi ya visababishi vikuu. Hakuna mbinu maalum lakini ni mjadala ambao lazima uje na mikakati iliyo ndani ya uwezo wa timu na mazingira ya timu ya maboresho kwa kutumia rasilimali zilizopo. Kwa ile mizizi ambayo iko juu ya uwezo wa timu ya maboresho, basi iwasilishwe kwa ngazi za juu kwa msaada wa Mshauri (Mentor).

> ***Baada ya kupata mikakati, kinachofuata ni utekelezaji. Maana mikakati bila kutekeleza haiwezi kuleta matokeo.***

# HATUA YA SITA

## UTEKELEZAJI WA MIKAKATI YA MABORESHO

Kujua mikakati ya tatizo bila kufanya utekelezaji haina maana yeyote. Uzoefu unaonyesha hii ni shida ya timu nyingi za maboresho na hata pia watu binafsi. Wengi wanajua mizizi ya changamoto zao, mikakati ya utatuzi wanaifahamu, shida inakuwa kwenye utekelezaji. Zipo timu zisizotekeleza kabisa na zipo ambazo zinaanza bila kufikia mwishoni. Hatua hii ya 6 inatupa mbinu ya sayansi ya maboresho inayosaidia kuongoza timu ya maboresho kwenye kufanya utekelezaji wa mikakati ya maboresho.


**MBINU GANI?**

**HATUA 4 ZA MDUARA WA SAYANSI YA MABORESHO**

Kabla hatujaangalia hizi hatua 4 za mduara wa sayansi ya maboresho, yafaa kujifunza malengo makubwa ya mduara huu. Mduara huu lengo lake ni kutusaidia kuweza kujibu maswali 3 ya maboresho.

MASWALI 3 YA SAYANSI YA MABORESHO

1. **Ni jambo gani tunataka kufanikisha) (what are we trying to accomplish).**
   Maboresho yoyote yatakuwa na maana kama unajibu lilowazi kichwani mwako kwamba, mwisho wa mambo yote unataka kufanikisha jambo gani? Hii ni muhimu sana kukusaidia kujua kama mikakati yako inajibu hili swali ama la.





2. **Tutajuaje kama mabadiliko yaliyotokea ni Maboresho (How will we know that a change is an improvement?)**
   Hii ni muhimu sana. Kwa sababu sio kila mabadiliko ni maboresho. Lengo la timu ya maboresho ni kuleta mabadiliko yatakayoleta tija. Kama timu lazima kujiuliza, tutajuaje kama mabadiliko yatakayotokea ni maboresho?

   Mbinu inayotumika ni kuangalia takwimu na kuchora graph inayoonesha matokeo ya mabadiliko. Endapo mabadiliko yanaonesha maboresho, hii ina maana mikakati inafanya vema, na kama mabadiliko hayaonyeshi maboresho, hapo yafaa kukaa tena kama timu na kutafuta mikakati mingine.


3. **Ni jambo gani tukilifanya litaleta maboresho? (What change will bring improvement)**
   Kama timu ya maboresho, tunalazimika kuweza kusema ni kitu gani tulikifanya kitaleta maboresho yenye tija. Kujua hili itategemea sana takwimu zetu na graph imeonyeshaje. Kama graph yetu imeonyesha maboresho, hapo tutajua ule mkakati tuloutumia umezaa matunda hayo ndio umetuletea maboresho.

**HAYA SASA TUANGALIE HATUA ZILE NNE ZA MDUARA WA SAYANSI YA MABORESHO**





1. **Panga (Plan):** Panga jaribio, ikiwemo mpango wa kukusanya takwimu.

- Eleza swali unalotaka kujibu na fanya makadirio kuhusu ni kipi kitatokea.
- Tengeneza mpango wa kufanya jaribio la mabadiliko (Nani atafanya nini- kugawana majukumu? Nini kitafanyika? Lini – (timeline)? Wapi?)
- Ainisha ni takwimu zipi utahitaji kuzikusanya





2. **Tekeleza (Do):** Tekeleza jaribio katika eneo dogo

- Tekeleza jaribio
- Weka kumbukumbu ya changamoto na matokeo yasiyotarajiwa katika kipindi cha majaribio
- Kusanya na anza kuchambua takwimu




3. **Tathmini (Study):** Chambua matokeo na linganisha na makadirio yako

- Kamilisha uchambuzi wa takwimu ikiwezekana kwa pamoja katika timu
- Linganisha takwimu na makadirio yako
- Fanya hitimisho na angalia ulichojifunza




4. **Chukua hatua (Act):** Kutegemea na ulichojifunza katika jaribio, tengeneza mpango wa hatua inayofuata.

- **Kama jaribio lilikuwa na mafanikio**

  **a)** Endeleza utekelezaji eneo la sasa pia tekeleza katika eneo kubwa zaidi
  **b)** Waeleze uzoefu wako wadau wengine wapate kujifunza
  **c)** Andaa mpango mwingine ( PDSA) – kutatua changamoto nyinginezo

- **Kama jaribio halikuwa na mafanikio**

  a) Sitisha jaribio
  b) Buni jaribio lingine kwa kuanzia eneo dogo